# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI

**SHULE YA SEKONDARI MZENGA,**
**S.L.P 28021,**
**KISARAWE – PWANI.**

**KATA YA VIHINGO**
**SIMU NA: +255752885600 MKUU**
**SIMU NA: +255784349349 MAKAMU**
**Email: mzengasec@gmail.com.**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZENGA**

**KIDATO CHA TANO 2024/2025.**

Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi (Majina matatu) **…….…………………………………...……………**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ni miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Mzenga kwa mwaka 2024/2025.
Ninampongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii, Hongera sana! Ni matumaini yangu kuwa ataipokea kwa furaha na kuitumia nafasi hii kujiendeleza kielimu kwa manufaa yake binafsi, familia yake na taifa kwa ujumla.

Yafuatayo ni mambo anayotakiwa kuyatimiza kabla ya kujiunga na shule ya Sekondari Mzenga; -

1. **KUFUNGUA SHULE.**

Shule itafunguliwa rasmi mnamo tarehe **01.07.2024**, naye anatakiwa kufika mnamo tarehe **30.06.2024** siku ya **Jumapili** tayari kuanza masomo mnamo Tarehe **01.07.2024** saa mbili kamili asubuhi. Na mwisho wa kuripoti ni Tarehe **31.07.2024**
Kutokufika shule kwa muda huo ni kosa na utakuwa umepoteza nafasi hiyo, hivyo basi zingatia kufika kwa wakati ili ukamilishe usajili.

2. **MAHALI SHULE ILIPO.**

Shule ya Sekondari Mzenga ipo katika kata ya Vihingo, tarafa ya Mzenga, kando kando mwa barabara itokayo Mlandizi kwenda Maneromango. Jinsi ya kufika shuleni: Watakao pita Barabara ya Morogoro, washuke Mlandizi na waulizie standi ya magari yanayoelekea Mzenga. Kutoka Mlandizi hadi Mzenga Sekondari ni **25km** na shule ipo kando ya Barabara, na nauli kwa gari **Tsh. 3,000/=** na pikipiki ni **Tsh. 6,000/=** Atakaotokea **Dar es Salaam, Gongo la Mboto,** atapandia gari stendi ya **Kigogo-Chanika,** na atashukia Mzenga A, nauli ni **Tsh. 7,000/=** na kuchukua bodaboda na kuomba apelekwe Mzenga Sekondari, nauli **1,000/=** tu.

3. **FOMU YA KUKUBALI KUANDIKISHWA.**

Fomu hii uijaze kwa kushirikiana na mzazi/ mlezi wako kwa kuzingatia maelezo yaliyopo kwenye fomu na uje nayo siku ya kufika shuleni.

4. **FOMU YA KUPIMWA AFYA**

Ijaze fomu hiyo na uipeleke kwenye **Hospitali ya Serikali** na mganga akupime na kukujazia taarifa zote kama zilivyooneshwa kwenye fomu. Fomu hiyo uje nayo shuleni siku ya kuripoti shuleni.
**NB:** Fomu hiyo ijazwe kwenye hospitali za serikali au kituo cha afya na si vinginevyo.

5. **VIFAA VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA KUJA SHULENI.**

1) Madaftari Makubwa **7** QUARE 3.
2) Kalamu za Wino 4 (blue au nyeusi) na Kalamu za Risasi 2 (penseli) aina ya HB.
3) Seti ya Vifaa vya Hisabati 1 (Mathematical Set) kwa wataosoma somo la Geography.
4) Bunda mbili za Karatasi, moja (**Ream A4** aina ya **Smart Copy)** na moja ya mistari **(Ruled)** kwa ajili ya mitihani ya mara kwa mara.
5) File la kuwekea taarifa za mwanafunzi. Ni lazima. (***la Transparent***)
6) Picha mbili za passport size za Mwanafunzi na mbili za Mzazi au Mlezi.

## 6. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

(a) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika orodha imeambatanishwa mwishoni mwa fomu hii.
(b) Scientific Calculator; kwa wataosoma somo la Geography.
(c) Godoro futi *(2½)*.
(d) Mashuka Jozi 2 rangi ya pink (kwa wasichana) na light blue (kwa wavulana), blanket 1, foronya ya godoro 1 rangi ya shuka lako, chandarua 1 cha pembe 4 rangi nyeupe size ya godoro.
(e) Nguo za ndani za kutosha;
(f) Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe ziwe za mfupa zisiwe za mpira (plastic) , kijiko na chupa ya kuhifadhia maji ya kunywa
(g) Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na kubwa moja (lita 20) yenye mfuniko
(h) ***Kwanja 1***, ***jembe 1***, ***reki 1***, ***mifagio 2*** wa ndani, ***mfagio 1*** wa nje wenye mpini mrefu, ***panga 1, mfagio mgumu mkubwa*** na mdogo wa kusafishia sakafu ya chooni, na ***sqeezer*** kwa ajili ya kusukumia maji wakati wa usafi na sabuni ya maji lita 5 kwa ajili ya usafi chooni.

7. **MICHANGO MBALIMBALI**
**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Michango ilipwe Benki ya NMB tawi la Kisarawe au tawi lolote la NMB nchini kwa akaunti namba **21401100005** jina la akaunti ni**: MZENGA SECONDARY SCHOOL.**

## 8. Viambatisho na Fomu Muhimu

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
(b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
(d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
(e) Picha (passport) za mwanafunzi atapiga shuleni.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## 9. MAVAZI RASMI YA SHULE.

***WAVULANA***

a) Shati Nyeupe yenye mikono mirefu jozi 2.
b) Suluari za **Kijivu (Escot Grey)** jozi 2, ziwe na rinda mbili na chini nchi 16 Upana.
   Kuvaa modo (model) au Mlegezo ni Kosa, ***HUTAPOKELEWA*** ukiwa umevaa mlegezo au modo.
c) Viatu Vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba jozi 2 (**Gidamu**) na visiwe na visigino virefu vya kupiga kelele sakafuni.
d) Bukta moja ya rangi yoyote na Fulana ya rangi ***yoyote, isiwe na maandishi*** kwa ajili ya michezo.
e) Soksi za Rangi Nyeusi pair 3.
f) Fulana zenye kola, za rangi ya **Kijivu (Escot Grey)** 2 (form six) kwa ajili ya darasani siku ya ***Jumatano na Ijumaa.*** Ni lazima kwani ni sare ya shule.
g) Sweta za rangi ya Kijivu **(Escot Grey)** 2 zenye umbo la **V-shingoni**. ni sare zitavaliwa wakati wa baridi.
h) Shamba Dress (nguo za kushindia) ni suluari Nyeusi 2 na T-shirt 2 za **Kijivu (Escot Grey)** zenye kola.
i) Sare zote lazima ziwe na nembo ya shule, itapatikana shuleni.
j) Track Suit ya **Kijivu (Escot Grey)** kwa ajili ya preparation.

***WASICHANA.***

(a) Shati Nyeupe yenye mikono mirefu jozi 2.
(b) Sketi za **Kijivu (Escot Grey)** jozi 2, ziwe na mshono wa umbo la V na ziwe ndefu zivuke magoti.
(c) Viatu Vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba jozi 2 (**Gidamu**) na visiwe na visigino virefu vya kupiga kelele sakafuni.
(d) Bukta moja ya rangi yoyote na Fulana ya rangi ***yoyote, isiwe na maandishi*** kwa ajili ya michezo.
(e) Soksi za Rangi Nyeupe pair 3 au zaidi.
(f) Fulana zenye kola, za rangi ya **Kijivu (Escot Grey)** 2 (form six) kwa ajili ya darasani siku ya ***Jumatano na Ijumaa.*** Ni lazima kwani ni sare ya shule.
(g) Sweta za rangi ya Kijivu **(Escot Grey)** 2 zenye umbo la **V-shingoni**. ni sare zitavaliwa wakati wa baridi.
(h) Shamba Dress (nguo za kushindia) ni Sketi Nyeusi 2 na T-shirt 2 za **Kijivu (Escot Grey)** zenye kola.
(i) Sare zote lazima ziwe na nembo ya shule, itapatikana shuleni.
(j) Track Suit ya **Kijivu (Escot Grey)** kwa ajili ya preparation.

### *Sheria na Kanuni muhimu za Shule*

*Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;*

## 10. SHERIA ZA SHULE

### Mambo ya kuzingatia:

Shule ya Sekondari Mzenga ni mahali panapoishi walimu, Wafanyakazi wasio Walimu na Wanafunzi. Hivyo inatakiwa kutambuana na kuheshimiana.

## 11.HESHIMA

a) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
b) Kusimama na kumsalimu mwalimu, mzazi au kiongozi anapoingia darasani au kwenye maeneo ya shule na nje ya shule.
c) Kutumia LUGHA NZURI ya heshima mahali popote kwa mtu yeyote.
d) Kuheshimu ***Bendera ya taifa***, ***Picha ya viongozi*** wa nchi, ***Nembo ya taifa*** (Court of Arm), Fedha na Wimbo wa taifa. ***(National Symbols)***
e) Kuheshimu ofisi za shule, ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, mali za umma na mali binafsi zilizopo katika mazingira ya shule.
f) Kusimama kwenye mstari wakati wa kupokea huduma.
g) Mwanafunzi akimbie na kuwahi anaposikia wito wa dharura (Kengele).
h) Kukubali na kuheshimu tofauti za ***KIDINI, KIJINSIA, KISIASA NA KIUTAMADUNI*** katika jamii. Mwanafunzi haruhusiwi kuhubiri dini, siasa au jambo lolote shuleni. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile kanisani, msikitini na katika vipindi vya dini vilivyopangwa kwenye ratiba ya shule.

## 12.RATIBA YA SHULE.

Mwanafunzi awepo shuleni saa KUMI NA MBILI NA NUSU asubuhi. Mwanafunzi anatakiwa kukaa darasani muda wote wa vipindi na kutimiza wajibu na kazi alizopewa kwa siku hiyo.

## 13.MIPAKA YA SHULE

Mwanafunzi aifahamu vizuri mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu kuwepo ndani ya mipaka hiyo au nje ya mipaka hiyo kwa kibali maalum kutoka kwa **MKUU WA SHULE** wakati wote. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea/kuingia kwenye nyumba za starehe, vilabu vya pombe na nyumba za kufikia wageni.

14. **USAFI**

a) Kutunza usafi wa mwili; Nywele fupi njiti ya kiberiti isinase, mkato wa kawaida bila mtindo wowote.
b) Mwanafunzi haruhusiwi; kusuka nywele kutinda nyusi, kupaka wanja, kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kufuga mustachi au ndevu, kuvaa bangili, hereni, mikufu, pete, au urembo wowote.
c) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule wakati wote anapokuwa katika mazingira ya shule na katika mikusanyiko maalumu ya kitaifa na kishule. Sare zivaliwe vizuri wakati wote, Shati/ Tshirt lichomekewe vizuri ndani ya suruali /sketi.
d) Mwanafunzi atakaye vaa sare ya shule isiyokidhi vipimo vilivyoelekezwa na shule, ataadhibiwa na atalazimika kushona /kununua nyingine.
e) Mwanafunzi anatakiwa kutunza mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo, kutotupa ovyo takataka za aina yoyote darasani au nje ya darasa, kutokatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.
f) Mwanafunzi haruhusiwi kubandika tangazo lolote katika kuta za mbao za matangazo za shule bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.

**15. MAHUDHURIO**

**a)** Mwanafunzi ambae hatahudhuria masomo kwa zaidi ya siku mbili (2) mfululizo kwa sababu yoyote ile, haruhusiwi kuhudhuria masomo mpaka apate kibali kutoka ***IDARA YA TAALUMA***. Vile vile mwanafunzi ambae hatahudhuria masomo kwa jumla ya siku tano (5) bila taarifa kabla ya mtihani wowote wa shule, hataruhusiwa kufanya mtihani huo hadi taarifa itoke kwa ***MKUU WA SHULE.***

**b)** Kila mwanafunzi anawajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo pamoja na kipindi cha dini.

**16. SIMU NA VIFAA VYA KI-ELECTRONIKI**

Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kutumia simu au kifaa chochote cha electronic akiwa shuleni. Mwanafunzi akikamatwa na simu, Ipod au kifaa chochote cha electronic kisichoruhusiwa ataadhibiwa na kifaa kitachukuliwa na kuharibiwa papo hapo.

17. **MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

a) Makosa ya jinai
b) Uasherati, ubakaji na ushoga au viashiria vinavyoonesha Uasherati, ubakaji na ushoga.
c) Ulevi, uvutaji bangi, na matumizi ya dawa za kulevya
d) Kupiga au kupigana na mwanafunzi mwenzie, mwalimu, mfanyakazi au mtu yeyote
e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
f) Kudharau bendera ya taifa
g) Kuoa au kuolewa
h) Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
i) Kugoma, kuchochea,au kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
j) Kukataa adhabu halali inayotolewa baada ya kufanya kosa.
k) Kushiriki, matendo uhalifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
l) Utoro wa rejareja na uliokithiri.

**18. MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI WAKATI WA USAJILI**

**a)** Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali au kituo cha afya, fomu hii itakabidhiwa kwa Mwalimu anayepokea Watoto au Makamu mkuu wa shule mara tu atakaporipoti shuleni mwanafunzi.
**b)** Fomu ya mzazi kukiri/kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
**c)** Nakala ya kivuli ya cheti cha kuzaliwa mwanafunzi.
**d)** Nakala ya matokeo ya kidato cha nne **(Result Slip).**
**e)** Bima ya afya, ni muhimu kuja nayo.

**NB:** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***19. MAPOKEZI.***

Ufikapo shuleni ulizia mahali wanaposajiliwa wanafunzi au ofisi ya Makamu Mkuu wa shule, siku ya kuja, uje ukiwa umetimiza maagizo yote kama ilivyoelekezwa hapo juu.

Nakutakia maandalizi mema. Na kwa mara nyingine, **Karibu shule ya Sekondari Mzenga.**

## *MOTTO WA SHULE.*

**Motto** wa shule ya Sekondari Mzenga ni *“ELIMU KWANZA”*
Zingatia motto huo kwa kusudi lililokuleta hapa shuleni.

...........................................

***Hassan R. Rusheye,***
***MKUU WA SHULE.***

# ORODHA YA VITABU

**SOMO LA GEOGRAPHY**

1. Physical Geography by TIE.
2. Practical Geography by TIE.
3. Principles of Physical Geography by F J monk house
4. Geography Integrated Approach by D. waugh
5. Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
6. General Geography in Diagram by R B burnet
7. Simplified Physical Geography(A-LEVEL) by D M
8. Statistical Methods and the Geographers by S. Gregory

**SOMO LA HISTORY**

1. Advanced level History 1 by TIE.
2. Advanced level History 2 by TIE.
3. Advanced learners, History form V and six (history 1 and 2) (oxford 2011)
4. Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to present (zist Kamili 2010)
5. Major events in the world History
6. Advanced level History (Nyambari nyangwine 2007
7. Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012

**SOMO LA ENGLISH LANGUAGE NA LITERATURE IN ENGLISH**

1. English for Advance Level, Phonology, Stylistics
2. English for Advance level by TIE.
3. **Novel:** The Beautiful ones are not yet born, A man of the People, Divine Providence, His Excellency the Head of State, A season of Waiting, The Rape of the Pearl, Encounters from Africa
4. **Poetry:** Selected Poems, The Wonderful Surgeon and other Poems
5. **Plays:** an enemy of the People, Black Mamba, I will Marry When I want, Betrayal in the City, The Bride, Lwanda Magere

**SOMO LA KISWAHILI NA FASIHI YA KISWAHILI**

1. **Kiswahili kwa ajili ya kidato cha Tano na Sita by TIE**
2. Sarufi Muundo ya Kiswahili (SAMIKISA)
3. Fasihi  na Sarufi Sekondari na Vyuo
4. **Riwaya**: Vuta n'Kuvute, Mfadhili, usiku utakapokwisha, Kufikirika, Mfadhili.
5. **Tamthiliya**: kwenye ukingo wa thim, Morani, Kivuli Kinaishi, Nguzo Mama
6. **Ushairi**:  Kimbunga, Chungu Tamu.Mapenzi Bora, Fungate ya Uhuru

**SOMO LA GENERAL STUDIES**

1. General studies for A- Level by TIE
2. 1.General studies for A- Level certificate form v
3. 2.Contemporary approach for A level general studies notes for form v and six
4. 3.General studies supplementary book for A level and colleges

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

# Shule ya Sekondari Mzenga

**FOMU YA KUKUBALI KUANDIKISHWA SHULENI KIDATO CHA TANO 2024/2025**

.

PICHA YA MWANAFUNZI PICHA YA MZAZI/MLEZI

**(Ijazwe na kurudishwa shuleni)**

**SEHEMU A: MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………………………………..
2. Tarehe ya kuzaliwa………………Mwezi………….Mwaka…………..……..
3. Wilaya uliyozaliwa…………………………………. Mkoa…………………………………
4. Uraia……………………………………………… Dini……………………………………..
5. Shule ya Sekondari uliyotoka……………………………… Daraja la ufaulu: ……… Alama ……..

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Naikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga kidato cha Tano katika **Shule ya Sekondari Mzenga.** Ninaahidi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuhudhuria masomo na kujifunza kwa bidii, kufanya kazi nyingine kwa juhudi na maarifa pamoja na kutii kikamilifu sheria na kanuni zote zilizowekwa na shule pamoja na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wote niwapo mwanafunzi wa shule hii.

Sahihi ya Mwanafunzi………………………………………. Tarehe…………………………

**SEHEMU B: MZAZI / MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi /Mlezi…………………………………………………………..……..
2. Kama ni mlezi taja uhusiano wako na mwanafunzi…………………………………….….……
3. Mahali unapoishi…………………………………………………………………...…….
4. Namba ya simu inayopatikana muda wote: ………………………………………………..

**AHADI YA MZAZI / MLEZI**

Nawajibika kwa mwanafunzi mtajwa hapo juu**.** Nitahakikisha kuwa kijana wangu anahudhuria siku zote za masomo na shughuli nyingine kama inavyotakiwa. Pia nitashirikiana na uongozi wa shule katika kufuatilia na kuhakikisha maendeleo ya kijana yako vizuri muda wote akiwa mwanafunzi.

**Sahihi ya Mzazi / Mlezi**……………………………… **Tarehe:** …………………………

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT - RALG
KISARAWE DISTRICT COUNCIL

# Mzenga Secondary school

**P.O.BOX 28021**
**KISARAWE - PWANI.**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

**To Medical Officer**

…………………………………………………………

…………………………………………………………..

…………………………………………………………

**Student Name………………………………………………………**

Please examine the above named student as to his / her fitness for appointment as a student. Comment on his / her health responding to the following items

A. Sight……………………………………………………………………………………………
B. Hearing………………………………………………………………………………………
C. Speech………………………………………………………………………………………
D. Blood pressure……………………………………………………………………………
E. Asthma………………………………………………………………………………………
F. T.B………………………………………………………………………………………………
G. Stool examination………………………………………………………………………
H. Any physical disability/Impairment……………………………………………………
I. Pregnancy (**Girls only**) ……………………………………………………………………

I have examined the student and consider that he/she is physically fit/unfit to pursue school activities.

Signature…………………………………………………… Date……………………………………..

Designation……………………………………………… Station stamp…………………………